Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

Swaum Ya Mwezi Wa Ramadhaan Kama alivyotekeleza Mtume (صلى الله عليه وسلم)

[Sheikh Ali al-Halabi na Sheikh Saleem al-Hilaali]

3rd Ramadhaan 1431
13th August, 2010

Volume 1, Issue 2

Fadhla za Swaum

Aya zenye kudhihirika wazi katika kitabu kitakatifu cha Allaah zinahimiza kufunga kama njia ya mja kutafuta kujikurubisha na Allaah (سبحانه وتعالى) na kuzifafanua fadhla zake, k.m kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

"Bila shaka wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanawake wanaozifuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanaume wanaoziamini vizuri nguzo za Imani, na wanawake wanaoziamini vizuri nguzo za Imani, na wanaume wanaotii, na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli, na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri, na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea, na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa (Zaka na) Sadaka, na wanawake wanaotoa (Zaka na) Sadaka, na wanaume wanaofunga, na wanawake wanaofunga, na wanaume wanaojihifadhi tupu zao, na wanawake wanaojihifadhi, na wanaume wanaomtaja Allaah kwa wingi, na wanawake wanaomtaja Allaah (kwa wingi). Allaah amewaandalia msamaha na ujira mkubwa." [Al-Ahzaab 33:35]

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema:

"Na (huku) kufunga ni bora kwenu. Ikiwa mnajua (haya sasa basi fuateni." [Al-Baqarah 2:184]

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amefafanua katika Sunnah iliyothubutu yakwamba kufunga ni kinga ya matamanio, kinga ya moto, na kwamba Allaah ameuweka makhsusi mmojawapo wa milango ya peponi kwa ajili yake. Itaiongoza nafsi mbali na matamanio yake, na kuiepusha na yale mambo ambayo ilikuja kugundua yakwamba yalikuwa ni ya kujistarehesha, ili ipate utulivu. Malipo haya makubwa na baraka nyingi yameelezwa kwa uzuri kikamilifu katika hadeeth ifuatayo iliyo saheeh.

Swaum ni Kinga

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amemuamrisha mtu mwenye matamanio na haja ya kuowa, lakini akawa hana uwezo wa kuowa, afunge. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaitangaza hatua hiyo kama njia ya kuyakata matamanio, kwani hupunguza, hutuliza na kudhibiti nguvu za viungo vya kiwiliwili. Imethibitishwa yakwamba jambo hilo lina athari kubwa katika kuhifadhi viungo na sehemu za ndani za mwili, hapo ndipo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema:

"Enyi mabarobaro, yoyote mwenye uwezo wa kuowa na afanye hivyo, kwani (huko kuowa) kutamfanya aangushe macho yake na kulinda tupu yake, na Yule asiyekuwa na uwezo, basi na afunge kwa sababu ni ngao yake."

Pia Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametupasha habari jinsi pepo ilivyozungukwa na mambo magumu na kwamba moto umezungukwa na matamanio. Kwahivyo unapojua, ewe Muislamu, yakwamba swaum hudhibiti nguvu za matamanio na kupunguza makali yake, na kwamba ni mambo haya ambayo yenye kumpeleka mtu motoni, basi utajionea jinsi swaum inavyokuja baina ya mja aliyefunga na moto. Kuna ahaadeeth zilizo wazi zinazoeleza yakwamba swaum ni kinga ya moto, na ni ngao ambayo mja huwenda akaitumia.

Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Hapana mja yoyote anayefunga kwa ajili ya Allaah, isipokuwa Allaah atauweka mbali uso wake na moto kwa umbali wa miaka sabiini kwa ajili hiyo."

Kisha akasema tena Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Swaum ni ngao ambayo mja hujikinga nayo na moto."

Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Yoyote mwenye kufunga siku mkoja kwa ajili ya Allaah, Allaah ataweka baina yake na moto shimo kiasi cha baina ya mbingu na ardhi."

Baadhi ya wanavyuoni wakashikilia msimamo yakwamba ahaadeeth hizi zilizotangulia zinahusu fadhila za kufunga haliyakuwa kwenye Jihaad katika njia ya Allaah. Hatahivyo, linalodhihirika ni kwamba kila swaum inayotekelezwa kwa ikhlaas, kwa kutarajia Uso wa Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyobainishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) *ni katika njia ya Allaah.*

Swaum husababisha mtu kuingia peponi

Ewe mja mtwi'ifu: Allaah akuafikie katika twa'a yako Kwake, na Akuwezeshe kutenda hayo, umekwisha kujua yakwamba swaum humuepusha mtu na moto na kwahivyo humsababisha kuwa karibu na pepo. Abu Umaamah (رضي الله عنه) amesema: "Nilisema kumwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Ewe mjumbe wa Allaah, niambie nami tendo ambalo litaniingiza peponi.' Akasema: *"Shikamana na Swaum, kwani hakuna mfano wake."*

Watalipwa Wenye Kufunga Ujira wao Pasi na Hisabu

Malipo makubwa yanamungoja yule mwenye kufunga, baada ya kupata furaha mara mbili – mara ya kwanza ni hapa ulimwenguni na mara nyengine ni katika siku ya malipo, na hata harufu itokayo kwenye kinywa chake ni bora mbele ya Allaah kuliko harufu ya misk. Abu Hurairah (رضي الله عنه) amesema; amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Amesema Allaah yakwamba vitendo vyote vya mwana-adamu ni vyake isipokuwa Swaum, kwani (hiyo swaum) ni kwa ajili yangu na mimi

(Endelea katika Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

Swaum	1-3
Mwezi Kongo	3
Matangazo	3
Ukumbi wa Kina mama	4

Nukta Muhimu za Mazingatio:

1. Kutakuwa na Darsa za wanawake katika mwezi wa Ramadhaan, msikiti wa Mazrui, kuanzia saa Nne asubuhi mpaka Adhuhuri—kila siku isipokuwa Ijumaa.
2. Jipatie Cd za Ustadh Na'maan kuhusu jinsi Älivyokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akifunga mwezi wa Ramadhaan. Na pia Cd za Mawaidha mbalimbali za ma-Duáat wetu.
3. Jipatie nakala ya vitabu vifuatavyo:

- Tafsiri ya Soorah Qaaf. [Sh. Nassor Khamis]
- Namna Ya Swala Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). [Sh. Al-Albaani]
- Damu Asilia Za Wanawake. [Sh. Ibn Uthaymeen]
- Na Risala nyenginezo zenye faida katika Dini.

Utayapata Yote hayo katika Maktaba ya QSS—Mombasa.

...Swaum Ya Mwezi wa Ramadhaan

(Kutoka Ukurasa wa 1)

ndiye nitakaemlipa. Na swaum ni kinga, na inapokuwa ndiyo siku ambayo mmoja wenu hufunga, basi na asizungumze maneno mabaya wala asigombane na mtu, na iwapo mtu yoyote atamtusi au atataka kupigana nae, basi na amwambie, 'Mimi nimefunga'. Naapa kwa yule aliyeimiliki nafsi ya Muhammad harufu itokayo kwenye kinywa cha aliyefunga ni bora kwa Allaah kuliko harufu ya misk. Kwa mwenye kufunga kuna nyakati mbili ya furaha; amalizapo kufunga hufurahi na atakapokutana na Mola wake atakuwa na furaha kutokana na kufunga kwake.'

Na katika riwaya iliyopokewa na al-Bukhaari kuna matamshi yasemayo:

"..Huwacha chakula chake na kinywaji chake na matamaniwa yake kwa ajili yangu Mimi, swaum ni yangu Mimi na Mimi ndiye nijuae nitakachomlipa mfungaji, na wema mmoja malipo yake ni mara kumi zaidi."

Na katika riwaya iliyopokewa na Muslim kuna matamshi yasemayo:

"Kila amali anayoifanya mwana-adamu hupewa nyongeza ya malipo, wema mmoja hulipwa mara kumi mfano wake, mpaka mara mia saba. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى), 'Isipokuwa kwa kufunga, kwani [Ibada hiyo] ni yangu na Mimi ndiye nijuae nitakachomlipa mfungaji, amewacha matamaniwa yake na chakula chake kwa ajili yangu.' Kwa mwenye kufunga kuna nyakati mbili za furaha; wakati wa furaha anapomaliza kufunga na wakati wa furaha atakapomuona Mola wake, na harufu itokayo kwenye kinywa cha mfungaji ni bora mbele ya Allaah kuliko harufu ya misk."

Swaum na Qur'aan zitamuombea kipenzi chao (mwenye kufunga)

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Swaum na Qur'an zitamshufa'iya mja siku ya kufufuliwa. Itasema Swaum: "Ewe Mola wangu mimi nilimzuiya na chakula na matamaniwa, nakuomba uikubali shifaa yangu kwake, na Qur'an itasema: Mimi nilimzuiya asilale wakati wa usiku, nakuomba uikubali shifaa yangu kwake, kwahiyo maombi yao yatakubaliwa."

Swaum ni fidia ya madhambi mbalimbali (Kaffaarah)

Miongoni mwa zile fadhla ambazo ni makhsusi kwa swaum ni kwamba Allaah amzifanya kuwa ni fidiya ya:

- Kunyoa nywele za kichwa haliyakuwa uko katika Ihraam kwa mwenye kufanya hivyo kutokana na ugonjwa.
- Mtu asoweza kutekeleza uwajibikaji wa kuchinja.
- Kumuuwa mtu bila ya kukusudia (kwa ajali) ambae mulowekeana nae mkataba.
- Kuwinda mnyama haliyakuwa uko katika hali ya Ihraam.
- Kuvunja kiapo.
- Dhihaar. (Mtu kumwambia mkewe, "Wewe ni kama mamangu.")

Yote haya yamechambuliwa katika Aayaat zifuatazo: Amesema Allaah (سبحانه وتعالى):

"Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Allaah. Na kama mkizuiwa, basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana. (Nao ni mbuzi). Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjoni mwao. (Napo ni hapo mahala walipozuiliwa). Na atakaekuwa mgonjwa katika nyinyi au ana vya kumuudhi kichwani mwake (akafanya yaliyokatazwa, kama vile kunyoa), basi atoe fidia kwa kufunga au (kwa kutoa) sadaka au kuchinja wanyama. Na mtakapokuwa salama, basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliyesahilika. (Naye ni mbuzi). Na asiyepata, afunge siku tatu katika hija na siku saba mtakaporudi (kwenu); hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu wa Makka. Na mcheni Allaah na jueni kuwa Allaah ni Mkali wa kuadhibu."

[al-Baqarah 2:196]

Akasema (جل ثناؤه):

"...Na (aliyeuawa) akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Muislamu; basi ampe uungwana mtumwa aliye Muislamu (basi; hapana wa kupewa diya). Na kama (aliyeuawa) ni mmoja wa watu ambao kuna ahadi baina yenu na baina yao; basi warithi wake wapewe malipo na pia apewe uungwana mtumwa aliye Muislamu. Na asiyepata basi afunge miezi miwili inayofuatana. Ndiyo kitubio kitokacho kwa Allaah. Na Allaah ni Mjuzi (na) Mwenye hikima." [an-Nisaa 4:92]

Akasema (السميع العليم):

"Allaah hatakuteseni kwa viapo vyenu vya upuzi, lakini atakukamateni kwa viapo mlivyoapa kwa nia mlioifunga baraa-bara. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha katikati mnachowalisha watu wa majumbani mwenu, au kuwavisha, au kumpa uungwana mtumwa. Lakini asiyeweza kupata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapoapa. Na vilindeni viapo vyenu, (msiape kisha msitimize). Namna hivi Allaah anakubainishieni Aya zake ili mpate kushukuru."

Akasema (العزيز الحكيم):

"Enyi mlioamini! Msiuwe mawindo na hali (yakuwa) mumo katika Hija au Umra. Na miongoni mwenu atakayemwua kwa kusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa (kuchinja) kilicho sawa na alichikiua, katika wanyama wanaofugwa, kama watakavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu mnyama huyo apelekwe iliko Kaaba (akachinjwe huko na kutasadakiwa masikini); au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake (hili). Allaah amekwishayafuta yaliyopita; lakini atakayefanya tena Allaah atampa adhabu. Na Allaah ndiye Mwenye nguvu (na) Mwenye kuadhibu."

[al-Maa'ida 5:95]

Akasema (الطيف الخبير):

"Na wale wawaitao wake zao mama zao, kisha wakarudi katika yale waliyoyasema, (wakataka kuwarejea wake zao wakae kama kidasturi ya mke na mume), basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana. Mnapewa maonyo kwa haya. Na Allaah anayajua (yote) mnayo yatenda. Na asiyepata (mtumwa) basi afunge swaum ya miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza, basi awalishe masikini sitini (kila maskini kibaba kimoja cha chakula kinacholiwa sana katika mahala hapo). (Mumeambiwa) haya ili mumuamini Allaah na Mtume wake; na hiyo ni mipaka ya Allaah, (msipindukie); na kwa makafiri iko adhabu iumizayo."

Vilevile Swaum, (Swala) na Sadaka huyafuta maovu yaliyosababishwa kwa mtu kwa kutokana na mali yake, jamii, na majirani. Kutoka kwa Hudhaifah Ibn al-Yamani (رضي الله عنه) aliyesema: Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Fitna ya mtu kwa watu wake, na mali yake, na jirani yake, kafara yake huwa ni swala kufunga na sadaka."

Ar-Rayyaan Ni Kwa Wale Wenye Kufunga

Kutoka kwa Sahl Ibn Sa'd (رضي الله عنه) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Kwa hakika kuna mlango wa peponi uitwao 'ar-Rayyaan'. Siku ya Qiyaama, wale waliofunga watauingia mlango huo; hapana yoyote atakaeuingia mlango huo isipokuwa wao, na watakapokuwa washaingia, utafungwa ili asiingie yoyote asiyekuwa katika wao, [kwahiyo atakapoingia wa mwisho wao, utafungwa, na yoyote aingiae atakunywa, na yoyote atakaekunywa hatoshikwa na kiu tena]."

Fadhla za Mwezi Wa Ramadhaan

Ramadhaan ni mwezi wa kheri nyingi na Baraka nyingi na Allaah akaubainisha kwa fadhla nyingi:

Ni Mwezi Wa Qur'aan

Allaah (عز وجل) ameteremsha Kitabu chake kitakatifu kuwa ni muongozo kwa watu na pozo kwa Waumini, kinacholingania katika yaliyo bora, na kubainisha njia ya sawa, na

(Endelea Katika Ukurasa wa 3)

...Swaum Ya Mwezi wa Ramadhaan

kiliteremshwa kwenye usiku wa *Lailatul-Qadr* katika mwezi wa Ramadhaan. Akasema (ذو العرش المجيد) Mwenye 'Arsh Mtukufu:

(Mwezi huo mlioambiwa mfunge) ni Mwezi wa Ramadhaan ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo hii Qur'an ili iwe uwongozi kwa watu, na hoja zilizo wazi wa uwongozi na upambanuzi (wa baina ya haki na batili). Atakayekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhaan) afunge ." [al-Baqarah 2:185]

Na ujue, ewe ndugu yangu, Allaah akubariki, yakwamba (katika aya ya hapo juu) kuhusiana na sifa ya mwezi wa Ramadhaan, na (taarifa) yakwamba Qur'aan iliteremshwa ndani yake, hufuatwa na kinachokuja baada ya herufi *faa* ambayo katika lugha ya kiarabu huashiriya madhumuni na sababu:

"Atakayekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhaan) afunge ." [al-Baqarah 2:185]

Hii inaashiriya yakwamba mwezi wa Ramadhaan ni mwezi wa swaum kwa sababu Qur'aan iliteremshwa kwenye kipindi hicho.

Kwenye kipindi hicho mashetani hufungwa, milango ya motoni hufungwa na milango ya peponi hufunguliwa

Kwahivyo shari hupungua katika ardhi uingiapo mwezi huu uliobarikiwa kwani majini waovu hufungwa kwa silisili, minyororo na pingu. Kwahiyo, hushindwa kuwapotosha watu kama wafanyavyo katika masiku mengine, kwani huwa Waislamu wakishughulika na swaum ambayo huvunja makali ya matamaniwa, na hujishughulisha na kusoma Qur'aan na vitendo vyengine vya 'Ibaada zenye kusafisha na kutakasa nyoyo.

[Endele katika makala yajayo]

MATANGAZO

Al-Rahma Hajj & Umrah Agencies

Kwa Safari ya Hajj, Al-Rahma Agencies, kutoka Mjini Mombasa, wanawatangazia Waislamu wote wenye niya ya kutekeleza Ámali hii Tukufu wajisajili katika afisi yao. Gharama za Safari ni $2,900.00 [US Dollars] - Kuanzia Mombasa mpaka Jeddah na Kurudi Mombasa; pamoja na Nyumba ya Kukaa [Makkah na Madinah] na Usafiri wa Ma-Bus. Na chakula [Mara Tatu kwa siku] katika siku za Mina kwa muda wa siku Tano. Msafara wetu Tutaandamana na Daktari [wetu] mpaka turudi nae Insha –Allaah. Darsa za maandalizi zitafanywa hapa [Mombasa] kabla ya kuondoka, na tukifika huko [Makkah].

Amma kwa upande wa kuchinja [udh-hiya] na chakula katika hoteli [Makkah na Madina] kila mtu ni juu yake. Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net au kwa kutupigia simu namba mojawapo ya hizi zifuatazo.

+254 723471820, au +245 721473181 au +254 700365253

(Endelea kuanzia Volume 1, Issue 1) **...Mwezi Kongo**

MUUNGANO WA MIPAKA: (MATLA')

Kutokamana na hadithi zilizopita, inampasa kila muislamu afuate amri kuhusu kuonekana kwa mwezi. Kwa kulikariri jambo hilo, ikapokewa kutoka kwa Abu Huraira, 'Aisha na wengineo (رضي الله عنها), Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:

"(Uhakika wa) Saum huanza ile siku muanzapo kufunga; (Uhakika wa) Fitr ('Idd) huwa ni ile siku mumalizapo kufunga; (Uhakika wa) Adh-ha ('Idd) huwa ni ile siku munapochinja."[10]

Kwa hivyo uonekanapo mwezi popote ulimwenguni na angalau muislamu mmoja muaminifu, hii yamaanisha ya kwamba umma mzima umeuona. Kutokamana na hayo, kama hadithi iliyopita inavyotuashiria juu ya kila muislamu kuwajibika kuupokea mwezi huo mpya, maadamu habari zitamfikia na wakati utamruhusu kuyatekeleza yanayompasa.

KUTOELEWEKA II: MATLA' TAFAUTI

Idadi kubwa ya watu wameipotoa riwaya ifuatayo ya Kurayb. Akatuhadithia Kurayb yakwamba Umm ul-Fadhl Bint ul-Harith alimtuma kwenda kwa Mu'awiyah (رضي الله عنه) huko Damascus. Baada ya kuutekeleza utumishi huo akiweko Sham, mwezi wa Ramadhani ukaandama usiku wa ljumaa jioni nae kurayb akauona. Kisha akarudi Madina na akawasili katika siku za mwisho mwisho wa mwezi. Akaonana na Ibn 'Abbas ambae akamuuliza ni lini mwezi wa Ramadhani ulipoandama huko Ash-Sham. Kurayb akasema "Tumeuona usiku wa ljumaa" Ibn 'Abbas akamuuliza "Je wewe mwenyewe uliuona?" akajibu Kurayb, "Ndio, nimeuona pamoja na watu wengine, na kwa ajili hiyo watu wakafunga pamoja na Mu'awiyah." Hapo tena Ibn 'Abbas akasema, "Lakini sisi tumeuona usiku wa ljumamosi, kwa hivyo sisi tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe siku thalathini au tuuone (mwezi kongo wa shawwal)." Kurayb akamuuliza, "Kwani wewe hukubali kuuona na kufunga kwa Ma'awiya?" Akajibu Ibn 'Abbas: "Laa! Hivi ndivyo tulivyoamrishwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (صلى الله عليه وسلم)."[11]

Baada ya majadiliano kuhusu riwaya hii, Shaykh-ul-Islam Ibn Taymiyyah (Rahimahullah) akamalizia:

"Kwa ufupi, yoyote itakaemfikia habari ya kuonekana kwa mwezi na akapata wasaa wa kufunga au kumaliza kufunga au kuchinja basi hana budi atekeleze. Ushahidi kamili na riwaya nyingi kutoka kwa Ma-Salaf unaunga mkono kikamilifu mas-ala hayo. Kuweka vipimo vya masafa au miji ni kukhalifu malengo na shar' (sheria ya uislamu)."[12]

Imam Ash-Shawkani (rahimahullah) akaigusia hii riwaya kutoka kwa Kurayb na akataja maoni mbali mbali ya wanavyuoni walivyozungumza. Kisha akaeleza kama ifuatavyo:

"Inakupasa kujua ya kwamba ushahidi unaokubalika ni kama alivyosema Ibn 'Abbas (رضي الله عنهما) waziwazi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Na sio katika ijtihadi yake, kama wanavyofasiri baadhi ya watu, wakati aliposema, 'Hivi ndivyo tulivyoamrishwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (صلى الله عليه وسلم).' Maelezo yake aliyoyapokea kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni yale yaliyonukuliwa na Al-Bukhari, Muslim na wengineo, walivyopokea ya kwamba: 'Musifunge mpaka muuone mwezi na musimalize saumu zenu mpaka muuone...'

Hii haihusiani na sehemu maalum bali hayo ni maelezo kwa waislamu wote kwa ujumla. Kwa hivyo huo ni ushahidi wa wazi ya kuwa kuonekana kwa mwezi katika sehemu moja kunawahusu watu wa sehemu yoyote nyingine. Sababu ni kwamba watu (waislamu) katika sehemu fulani wakiuona, hiyo yamaanisha kuwa waislamu wote wameuona; linalowahusu wao (waliouona) vile vile litawahusu wengine (katika sehemu nyingine.) Licha ya hayo, mji wa Ash-Sham haukuwa mbali mno kutoka Madina hata ipatikane matla' tafauti. Ibn 'Abbas alikataa kuwafuata waliouona. Hii yamaanisha tabia yake imetokamana na ijtihadi yake na kwa hivyo hauwezekani huo kuwa ni ushahidi (makhsusi)."[13]. (Endelea katika makala yajayo)

P. O. Box 85477,
Mombasa,

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفرقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net

Ukumbi Wa Wanawake

...Damu Asilia Za Kina Mama [Sheikh Muhammad bin Swaleh al-Uthaymeen] (رحمه الله)

(Endelea kutoka Volume 1, Issue 1)

Kwa hiyo, kwa vile hayakuthubutu haya makisio katika kitabu cha Allaah na katika Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلّم) inakuwa ni dhahiri yakwamba hayazingatiwi. Kwa hakika, mazingatio (kama yalivyothibitishwa hapo awali) huthibitishwa kwa kuwepo au kukosekana heidh. Kuna nukta ya faida muhimu sana inayopatikana kutokana na ithbati iliyopo kutoka katika mas'ala haya, nayo ni kwamba hukmu za Ki-Islamu haziwezi kuthibitishwa isipokuwa kwa dalili kutoka katika kitabu cha Allaah (Qur'an), na *Sunnah* za Mtume (صلى الله عليه وسلّم) au *Ijmaa'* ijulikanayo, au Qiyaas iliyo saheeh.

Amesema Sheikh Ul Islaam, Ibn Taymiyyah katika mojawapo ya hukmu zake za kimsingi: *"...na jina ni kama hilo:* ***Heidh****, Allaah amelifungamanisha kutokana nalo hukmu nyingi katika Kitaab na Sunnah na wala hakutupa "makisio" yake yanayofanya muda uwe ni mfupi au mrefu. Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلّم) hakubainisha wakati ambao mwanamke anapodhaniwa kuwa ni twahara baina ya miongoni mwa heidh zake mbili, hata kama Ummah umeathirika mno na suala hili na unahitaji kulijua. Ki-Lugha, hili neno Heidh halikuwa na tabia ya kutafautisha baina ya "makisio" ya heidh moja au nyengine. Kwahivyo, yoyote mwenye kukisia wakati maalum wa heidh, basi yeye; mume/mke; amechukuwa msimamo usolingana na Kitaab na Sunnah."*

Dalili No. 4:

Mazingatio yenye kumaanisha ulinganifu ulio thabiti na usio na hitilafu yoyote (kulinganisha kwa makadirio). Kwa vile Allaah (سبحانه وتعالى) ameipa heidh sifa ya madhara, kwa hivyo, pindi inapojitokeza, madhara yatadhihiri na hapatokuwa na tafauti yoyote iwapo itajitokeza katika siku ya pili au siku ya kwanza, siku ya 4 au siku ya 3, siku ya 16 au siku ya 15, siku ya 18 au siku ya 17 kwa sababu heidh ni heidh na madhara ni madhara. Sababu zitapatikana ndani ya masiku mawili yenye kufuatana sawa kwa kila mmoja. Kwahivyo, itaruhusiwa vipi kuhitilafiana katika hukmu baina ya masiku mawili ingawaje sababu zake ni moja? Jee, hayapingani hayo na ulinganifu wa sawa?

Kwani huo si ulinganifu wa sawa kwamba masiku yanatakiwa kuwa sawa katika hukmu kwa kuwa sawa kwa yenye kusababisha?

Dalili No. 5:

Ikhitafu na michafuko katika maneno ya wenye kutaja nyakati maalum za heidh zinaashiriya ukosefu wa dalili kwa maneno kama hayo. Rai hizi zilifikiwa kwa njia ya *Ijtihaad* na hutegemea mara nyengine kupata au kukosea na hakuna katika rai hizi lenye kupewa umuhimu wa kwanza kuliko jengine. Na itokeapo ikhtilafu mambo ni lazima yarudishwe kwenye Qur'an na Sunnah.

Kwahiyo, iwapo itadhihiri waziwazi yakwamba wazo la kukosekana mipaka ya nyakati fupi au ndefu ya heidh ni jambo lenye nguvu na lenye kupewa uzito zaidi kuliko mengine, basi itakubalika yakwamba damu yoyote ya asili inayomtoka mwanamke ionekanapo na mwanamke na ambayo haikusababishwa na kidonda au kitu chochote chengine itahesabiwa moja kwa moja kama damu ya heidh bila ya kuzingatia makisio yoyote ya nyakati au umri pale ilipotoka, isipokuwa kwamba damu itakayotoka kwa kuendelea bila ya kusita au itakayozuiwa kwa kiasi cha muda mchache tu kwa siku moja au mbili kwa kila mwezi. Damu kama hiyo itatambulika na kubainishwa kama damu ya **Istihaadhah** na yataelezwa baadae mbeleni pamoja na hukmu zenye kuhusika katika mlango wa 5.

Amesema Shaykh ul Islaam Ibn Taymiyyah: "*Kwa msingi kila kitu chenye kutoka katika uzao ni heidh mpaka dalili iweze kuthibitishwa kuashiria yakwamba ni* ***Istihaadhah.***" Pia alisema: "*Damu yoyote itokayo ni damu ya heidh isipokuwa iwapo itajulikana kuwa ni aina ya damu itokayo kwenye kidonda au ni damu itokayo kwenye mshipa wa damu.*" Licha yakuwa msemo huu ndiwo wenye nguvu zaidi lakini vilevile ndiwo ulio na mkuruba zaidi na ufahamu wenye mazingatio na ni wa rahisi zaidi kutekeleza. Inastahiki kukubalika kuliko rai zote nyengine kwa sababu inakubaliana na kiini na misingi ya ki-Islamu ambayo ni faraja na usahali.

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema:

"Na wala hakuwawekea katika Uislamu uzito wowote."

Mtume (صلى الله عليه وسلّم) amesema:

"Kwa hakika Dini hii ni rahisi sana na yoyote atakaejitweka katika dini yake hatoweza kuendelea namna hiyo. Kwahivyo musiwe washupavu, lakini jaribuni kuwa karibu na usawa na pokeeni bishara njema yakwamba mutalipwa malipo mema."

Na ilikuwa ni katika maumbile yake (صلى الله عليه وسلّم) pindi alipokuwa akikhiyari baina ya mambo mawili, yeye daima alikuwa akichagua lenye sahali au jepesi, isipokuwa iwapo litakuwa ni la makosa.

Heidh Ya Mwanamke Mwenye Mimba

Kwa mara nyingi, heidh husimama katika wakati wa mimba. Imaam Ahmad (رحمه الله) amesema:

"Wanawake wanaweza kutambua kuwa wamebeba mimba heidh zao zinaposimama."

Pindi mwanamke mwenye mimba anapoiona damu yake muda mchache kabla ya kuzaa (siku mbili au tatu) ikiandamana na uchungu wa mazazi, basi itazingatiwa kuwa ni **Nifaas.** Jee, (hiyo damu) ikitangulia kuonekana kabla ya kuzaa kwake au muda mchache tu kabla ya kuzaa lakini isiandamane na uchungu wa mazazi itazingatiwaje damu hiyo (ni heidh au la?) Hapa kuna ikhtilafu baina ya wanavyuoni kuhusiana na suala hili. Rai ya sawa, hatahivyo, ni kwamba aina hii ya damu ni damu ya heidh. Sababu ya yote hayo inapatikana katika hukmu ya ujumla kwamba "Damu inayomsibu (inayokabiliwa na) mwanamke ni damu ya heidh maadamu hakuna sababu yoyote yenye kubadilisha mazingatio yake kuwa ni heidh. Kwa maana hii, hakuna chochote katika Kitaab cha Allaah (Qur'an) na katika Sunnah kinachoashiria yakwamba haiwezekani kwa mwanamke mwenye mimba kuwa na heidh". Hii ndiyo rai ya Imaam Maalik, Imaam ash-Shaafi'ee, chaguo la Sheikh ul Islaam Ibn Taymiyyah, kama alivyosema katika *Al-Ikhtiyaraat, Uk. 30* na wala **sio Nifaas.** Katika hali hii, hwenda likaulizwa suali iwapo itaweza kuzingatiwa kuwa ni heidh na kwahiyo ipewe hukmu zote. Na vilevile imepokewa yakwamba Imaam Ahmad amechukuwa msimamo huwo. Kwa jinsi hali ilivyo, hukmu zote zenye muongozo wa heidh ya kawaida zinatumika kwa heidh ya mwanamke mwenye mimba **isipokuwa katika hali aina mbili:**

[Endelea katika makala yajayo]